JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU BUNDA

Simu:028-2621028
Fax:028-2621028
Mobile:0766633472/0787161792
Tovuti : www.bundatc.ac.tz
E-mail: bundattc@gmail.com

S.L.P 01
BUNDA - MARA
TANZANIA.

Kumb.Na BUNDA/TC/GF/VOL.IV/101/ 16/07/2018

MR/ MS _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA CHUO (JOINING INSTRUCTION) OKTOBA - 2018

Uongozi wa chuo unafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na **Stashahada ya ualimu wa Sekondari** katika chuo hiki. Mafunzo haya yatachukuwa muda wa miaka miwili (2). Unatakiwa kufika chuoni kuanzia tarehe **04/10/2018** na Usajili utaanza **04/10/2018** na utafungwa tarehe 1**3/10/2018** baada ya tarehe 1**3/10/2018** hautapokelewa wala kusajiliwa. Ni vema uwahi ili usipoteze nafasi yako hii adhimu pia upate maelekezo ya msingi katika mafunzo kabilishi **(Orientetions).** Mafunzo yataanza tarehe **15/10/2018**.

1. MAELEZO MAFUPI KUHUSU CHUO/MAFUNZO

Chuo kilianzishwa mwaka 1980 Wilayani Bunda Mkoani Mara. Bunda ni mahali pazuri na hata Chuo chetu ni kizuri pia. Moto au kauli yatu ni **"HEKIMA NA UMOJA" Dira ya Chuo chetu ni kutoa Elimu bora ya Ualimu kwa wanachuo Tarajali na mafunzo kazini.** Umbali kutoka Bunda Mjini ni km 2.5 barabara kuu iendayo Musoma/Tarime, shukia kituo cha mabasi cha **Nyasura Senta** ili kuepuka usumbufu. Aidha kila mwanachuo atasajiliwa kwenye mchepuo kwa kuzingatia masomo na tahasusi (combinations) atakayopangiwa kulingana na aliyofaulu.

2. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

(A) VITAMBULISHO VYA KUJA NAVYO

- Vyeti halisi vya kidato cha nne na sita au hati ya matokeo (Slip Results) kwa waliomaliza 2018.
- Score sheets hazitapokelewa.
- Cheti cha kuhitimu shule (school leaving certificate).
- Barua hii ya kukuita chuoni (Joining instruction).
- Vitambulisho vya shule au kitambulisho kingine kinachokutambulisha kama vile kitabu cha benki au **"passport" au cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha uraia.**
- Walioajiriwa wawe na vitambulisho vya kazi na barua ya ruhusa toka kwa mwajiri wao.

(B) MICHANGO / ADA

- Unatakiwa kulipa kwenye akaunti za Chuo zifuatazo michango/ ada. Usilete fedha taslimu chuoni. Njoo na risiti **(Bank pay-in- slips)** tu kwa uthibitisho na **ulipie bank na siyo kwa NMB wakala**. Inatakiwa lionekane jina la mwanachuo katika hati ya malipo **(Bank Pay-in-slip).** Ada ilipwe Rev. A/C **30101100012** NMB Bunda (kipengele (a) hapo chini.
- Michango yote iwekwe Miscellaneous Account: **No. 30103500086 NMB Bunda** (Vipengele c-m hapo chini). **Soma vipengele C -M kwa makini.**
- Fedha ya SEWATA iwekwe katika akaunti ya **SEWATA Akaunti No. 30102300789 NMB Bunda**. (**SEWATA** ni serikali ya wanachuo) kama ilivyoelekezwa katika kipengele (b)
- Malipo yafanyike kwenye **akaunti tajwa hapo juu kwenye tawi lolote la NMB na si vinginevyo**.

ADA

- Ada ya Mafunzo ni Tshs.600,000/= kwa mwaka (au una weza kulipa Tshs. 300,000/= kwa muhula)

MICHANGO

- Huduma ya kwanza **Tshs. 5,000**/= kwa mwaka.
- Bima ya Afya ya Taifa **Tshs**. **50,400/=** kwa wasio na bima ya Afya
- Usajili **Tshs 5,000/=** inalipwa mara moja mwaka wa kwanza
- Serikali ya Wanachuo**Tshs. 5,000/=** kwa Mwaka
- Kukodi godoro**Tshs 20,000/=** kwa Mwaka.
- Huduma nyingine **Tshs. 20,000/=** (kwa mwaka)
- Kitambulisho **Tshs 5,000/=** kwa Mwaka wa Kwanza
- Elimu ya Michezo **Tshs 10,000/=** kwa mwaka.
- Ulinzi Tshs **15,000/=** kwa mwaka.
- ICT/TEHEMA **Tshs 20,000/=** kwa mwaka
- T – Shirt yenye Nembo ya Chuo **Tshs. 15,000/=** inapatikana chuoni
- Taaluma **Tshs 50,000/=** kwa mwaka
- Usafi na miundombinu **Tshs 20,000/=** kwa mwaka
- Ada ya mtihani wa Taifa **Tshs 50,000/=** kwa Mwaka wa pili wa Taifa
- Mahafali mtajulishwa

(C) SARE YA CHUO

Sare ya Chuo. Utatakiwa kushona sare ya chuo, nguo maridadi, nadhifu yenye kuonesha haiba nzuri ya ualimu kama ifuatavyo:-

- **WANAUME**.

- Suruali mbili au zaidi za kitambaa cha suti rangi (dark blue).
- Mashati mawili au zaidi mikono mirefu ambayo yanapatikana chuoni, moja Tshs **10,500/=**
- Tai dark blue mpya.
- Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu.
- Tisheti moja **yenye Nembo** ya chuo inapatikana chuoni Tshs 15,000/=

NB, Usilete mitumba au suruali za kubana (modal).

- **WANAWAKE**.
  - Sketi mbili au zaidi za kitambaa cha suti rangi (dark blue) za kushona Linda boksi na sio mitumba. Inchi **7** kuvuka magoti isiwe na mpasuo. **Sketi za Vimini hatutazipokea.**
  - Shati mbili mikono mirefu ambayo yanapatikana chuoni.
  - Michoro iliyopo hapo chini inaelekeza jinsi ya kushona Sketi na Suruali.
  - Picha No.01 (Sketi) na Picha No. 02 (Suruali).

SARE KWA AJILI YA WANAFUNZI WA KIISLAMU MFANO HIJABU ZIELEKEZWE VYEMA

PICHA1



INCHI 7

SKETI- LINDA BOKSI

PICHA 2



SURUALI

3. MAVAZI YA MICHEZO:

Michezo ni sehemu ya maisha hapa chuoni. Hivyo huna budi kushiriki kikamilifu. Leta viatu vya raba, bukta na fulana (T-shirt rangi nyeupe ya real Madreed).

Lazima uwe na track suti ya **rangi ya bluu bahari (light blue).**

Wasichana wanaweza kuleta sketi fupi ya kuvalia juu ya bukta.

4. VIFAA MUHIMU VYA KUJA NAVYO CHUONI.

- **Shuka**- Njoo na shuka mbili nyeupe kwa ajili ya kujifunika na kutandika, neti na blaketi pia.
- Leta picha (03) passport size za rangi kwa ajili ya rekodi za Ofisi na kitambulisho chako.
- Picha ioneshe uso kwa mbele, masikio yote mawili na iwe na background ya rangi ya blue.
- Njoo na ndoo, sahani, kikombe, bakuli, kijiko kwa matumizi binafsi.
- Njoo na mifagio miwili mmoja aina ya chelewa na wa pili aina ya soft broom.

5. VIFAA VYA TAALUMA

- Kalamu za kuandikia za kutosha rangi nyeusi na blue.
- Magic markers kwa ajili ya kuchorea vielelezo vya kufundishia rangi nyeusi, nyekundu, bluu na kijani.
- Kumbukumbu za kila siku (portifolio) mafaili (10) na bahasha kubwa moja kwa ajili ya kutunzia vyeti.
- Ream ya karatasi **(double A) original zinapatikana chuoni** zenye **jarada la rangi ya bluu.**

6. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:

Stashahada ya ualimu wa Sekondari katika chuo hiki hutolewa katika Tahasusi zifuatazo ; HGL, HKL, na HGK kwa mgawanyo wa masomo mawili mawili (HG, EK, GE, HK, HE)

7. CHETI CHA DAKTARI:

- Ili kuthibitisha kwamba afya yako ni njema kwa ajili ya mafunzo haya inakupasa upimwe katika Hospitali ya serikali/Hospitali teule. Pia kumbuka kwamba chuo hakina uwezo wa kuwaweka wanachuo wajawazito. **Hivyo kama una hali kama hiyo usije.**
- Hairuhusiwi kuleta majiko,hita, friji ,t.v n.k.
- Utasajiliwa na jopo la wakufunzi ambao watahakikisha kila ulichoagizwa umekileta usipokuwa nacho hautapokelewa.
- Aidha unatakiwa kuja na fedha za matumizi binafsi kwa ajili ya matumizi madogomadogo.

NTENDE MATHIAS AMOLLO
KAIMU MKUU WA CHUO

KIAMBATISHO NA. 2

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

TO: The Medical Officer

From: .....
Teachers' College.

.....
.....

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2.Neuroses
3.Other serious diseases.

B: Blood Group

Date : .....

Signature.....
Official Stamp

****

PART B: **MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time teacher Education course.

- (a) Eye – sight.....
- (b) Hearing.....
- (c) Limbs.....
- (d) Speech.....
- (e) Leprosy.....

II. Neuroses.....
III. Other serious diseases.....
IV. pregnancy.....

Date:.....Signature.....
Official Stamp